JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA OFISI YA RAIS - TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA MVOMERO SHULE YA SEKONDARI LUSANGA

P.O. Box 150
Lusanga –Turiani
Morogoro – Tanzania
E-mail lusangasec1990@gmail.com

Phone: +255655738944
+255787738944

03/05/2021

MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI

…….

…….

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI LUSANGA KIDATO CHA TANO MWAKA 2021/2022

Ninayo furaha kukuarifu kwamba binti yako. ……. amechaguliwa kujiunga na Shule ya Sekondari Lusanga kuchukua masomo yafuatayo:-

(i) HGL ☐
(ii) HGK ☐
(iii) CBG ☐
(iv) PCB ☐

Binti yako atakuwa hapa kwa muda wa miaka miwili, kipindi hiki cha maisha ni muhimu sana katika malezi yake. Ili tuweze kumsaidia akue vizuri na awe na mwenendo bora, ni lazima wewe Mzazi/Mlezi pia uwe tayari kushirikiana na Uongozi wa Shule.

Wakati binti yako akiwa shuleni tutamuongoza na kumtunza awe na mwenendo wa kufaa, iwapo italazimu tutamrudi kwa kadri taratibu zinavyoelekeza. Kadhalika kila mwisho wa muhula tutakuletea ripoti ya maendeleo yake kitaaluma na kitabia pia. Tunategemea akiwa likizo utaendelea kumuongoza.

Iwapo italazimu tutafurahi ukituletea ripoti juu ya mwenendo wake akiwa nyumbani. Kwa njia hii na kwa ushirikiano huu tutaweza kumsaidia binti yako akue vizuri na kuishi maisha bora baadae.

BAHATI M. OMARY - **……**
MKUU WA SHULE

MKUU WA SHULE
SHULE SEKONDARI LUSANGA
S. L. P. 150, TURIANI

B: 1: MAHALI SHULE ILIPO.

Shule ya Sekondari Lusanga ipo Tarafa ya Turiani karibu na mji mdogo wa Madizini. Mji mdogo wa Madizini upo Km 100 kutoka Morogoro Mjini (stendi ya Msamvu). Shule ipo umbali wa Km 2 kutoka mji mdogo wa madizini.

II: NAMNA YA KUFIKA SHULENI:

Unaweza kufika mji mdogo wa Madizini ukitokea Morogoro Mjini (msamvu stendi) au Dares Salaam (Ubungo stendi). Ukiwa Ubungo uliza Mabasi ya kwenda Turiani (*KVC au BM COACH* au *WADIDI au ZEELAND*) na ukiwa Morogoro uliza ZEELAND,K.LTD, ZENJBAR au *KVC* Mabasi haya yatakufikisha hadi Mji mdogo wa Madizini Stendi ya Mabasi, ambapo utapata usafiri wa kuja shuleni ambao ni pikipiki/, kwa gharama ya Tsh: 1,000/= (kwa pikipiki) na 5,000/= (kwa Tax). Mwendo wa kutoka Ubungo hadi Mji mdogo wa Madizini ni masaa saba (7). Na mwendo kutoka Morogoro mjini (Msamvu standi) hadi mji mdogo wa Madizini ni masaa mawili (2).

Kwa wanaotokea njia ya Arusha/Moshi/Korogwe/Handeni, kuna magari ya moja kwa moja ambayo ni *KVC Safari* na *Mapenzi ya Mungu*, mwambie dereva akushushe kituo kiitwacho “Kwa Temu” (shule ya msingi Lusanga) simama kama unaangalia gari linakoelekea, mkono wako wa kulia utaiona barabara ya vumbi hatua kama 25 utaliona geti la Shule ya Sekondari Lusanga.

Na wale wanaotokea Dodoma kuna gari la moja kwa moja pia liitwalo *HC Safari*, kutoka Dodoma hadi mji mdogo wa *Madizini/TURIANI.*

C: KUANZA KWA MUHULA:

Wanafunzi wa kidato cha Tano wafike shuleni 03/07/2021, Kila mwanafunzi atatakiwa kufika siku hiyo bila kukosa. Mwanafunzi afikapo shuleni aripoti ofisi ya makamu mkuu wa shule kwa ajili ya kuonesha stakabadhi ya malipo ya benki, kupewa maelekezo mengine muhimu kama taratibu ya sare ya shule na kukaguliwa vifaa alivyoagizwa. Muda wa kuripoti ni saa 2:00 asubuhi mpaka saa 12:00 jioni. Mwanafunzi hatapokelewa wala kupatiwa huduma nyingine yeyote nje ya muda huo. (kumbuka kuzingatia masaa ya kuripoti).

D: VIAMBATANISHO:

1. Fomu ya kukubali masharti: Fomu hii ijazwe na Mwanafunzi pia na Mzazi/ Mlezi na kuikabidhi shuleni.
2. Kivuli cha cheti cha kuzaliwa
3. Kivuli cha result slip ya kidato cha nne
4. Uthibitisho wa afya: peleka fomu iliyoambatanishwa kwa Mganga Mkuu wa Mkoa au Wilaya SIYO ZAHANATI ili upimwe afya na fomu irudishwe shuleni. (shule itazingatia taarifa ya afya ya mwanafunzi iliyothibitishwa na Daktari)
5. KITAMBULISHO CHA BIMA YA AFYA (CHF/NHIF). Kama hana umkatie awe nacho au umpe fedha kiasi cha Tsh 50,400/= kwa mwaka, atasaidiwa kukipata ili apate huduma za matibabu kwa ubora.

E: SARE ZA SHULE;

E: 1: SARE ZINAZOPATIKANA SHULENI:

- Sketi 2 za shule zenye rangi ya kijani rinda box ziwe ndefu kabisa (ifike kifundo cha mguu).
- Sketi 2 za Shule za kushindia (dark blue) rinda za kawaida ziwe ndefu kabisa. (ifike kifundo cha mguu).
- T-Shirt (fulana) maalum (Rangi nyeupe)
- Nembo ya shule

- Kitambulisho
- Tai

E: 2: SARE ANAZOTAKIWA KUJA NAZO:

- Viatu vyeusi vya ngozi vyenye visigino vifupi visivyo na urembo wowote , vyenye kamba za kufunga mbele, matundu manne(4) hadi sita(6)
- Soksi jozi mbili (2) ndefu nyeupe zisizo na urembo wowote.
- Raba za Michezo
- Truck suit mbili, moja ya michezo na nyingine ya kusomea usiku (rangi ya blue bahari) yenye upana unaoridhisha na isiyo ya kubana. Pia iwe na mistari mitatu pembeni yenye rangi nyeupe.
- T-shirt ya kijivu ya kushindia yenye shingo ya duara, isiyo na kola wala vifungo, pia isiwe na maandishi wala urembo wowote.
- Mashati ya shule mawili (mikono mirefu kwa wanaovaa hijabu na mikono mifupi kwa wasiovaa hijabu). Hijabu inayokubalika ni ya halua nyeupe yenye urefu unaofika kiunoni.
- Sweta rangi ya kijani iliyokolea.
- Shuka 2 zisizo na urembo (moja rangi ya blue bahari na nyingine rangi ya pink)
- Neti ya mbu nyeupe (pembe nne)
- Kwa wanaovaa hijabu wanaweza kuja na mitandio miwili kwa ajili ya kushindia yenye rangi nyeupe.
- Aje na brazia mbili (2) au vest mbili (2) nyeusi au nyeupe zisizo na maandishi, mishono au urembo wowote.

F**: MAHITAJI YA BWENINI ANAYOPASWA KUJA NAYO:**

- Godoro futi mbili na nusu upana, Urefu futi 6 na unene inch 4 au 6 lenye foronya ngumu.
- Ndala
- Kiwi, dawa ya meno na mswaki.
- Sabuni za kuogea na kufulia
- Taulo
- Taulo za kike za kujihifadhi
- Kanga au kitenge vya kuogea (doti mbili)
- Mwenye kitambulisho cha Bima ya afya aje nacho kitamsaidia.(*Mchango wa matibabu ni kwa ajili ya kununua dawa baridi na dharura tu*)
- Vyombo vya chakula; kikombe, Sahani, bakuri, kijiko (*visiwe cha plastiki*), na Chombo cha kubebea maji ya kunywa.
- Ndoo mbili ndogo za kufulia na kuogea.

MUHIMU:

NI MARUFUKU MWANAFUNZI KUJA NA NGUO AMBAZO SI SARE YA SHULE (NGUO ZA NYUMBANI)

G: MAHITAJI YA DARASANI ANAYOPASWA KUWA NAYO.

- Kalamu za kutosha
- Daftari kubwa za kutosha (Counter book) 3quire au 4 quire
- Penseli za kutosha
- Mkebe wa vifaa vya Hisabati
- Scientific Calculator **f(x) 991. CASIO** } wanaosoma sayansi
- Dissecting kit - wanaosoma Sayansi } **lazima**
- Dissecting tray – wanaosoma sayansi

- Laboratory coat (nyeupe) -wanaosoma sayansi - Graph paper –kwa wanaosoma Basic Applied Math's
- Advanced Learners Dictionary

MUHIMU: Vitabu vya masomo ya mchepuo husika angalau kimoja au viwili kwa kila somo na vitakaguliwa pindi tu atakaporipoti shuleni

H: VIFAA ANAVYOPASWA KUJA NAVYO NA KUKABIDHI SHULENI

• RIM YA KARATASI A4 NYEUPE MBILI (2) KWA MWAKA • NDOO 1 YA LITA 10

MCHEPUO	**AINA YA VIFAA**
HGL	Jembe +mpini +Soft broom
HGK	Reki+Squizer +Toilet brush
CBG	Slesha+ Squizer + Cobweb remover
PCB	Soft broom +Hard broom +Slesha

NB: Vifaa hivi pia vinapatikana kwenye duka la shule, unaweza kuja kununulia shuleni.

I: MAHITAJI YAFUATAYO YANAPATIKANA NA KULIPIWA SHULENI.

1	Sketi mbili za kijani	44,000/=
2	Sketi mbili za dark blue	44,000/=
3	Nembo mbili	5,000/=
4	T.Shirt (fulana) maalum	12,000/=
5	Tai	5,000/=
6	Picha na Kitambulisho	7000/=
	JUMLA	**117,000/=**

J: MAHITAJI YANAYOLIPIWA BENKI:
NMB AKAUNTI NAMBA 22001200012- LUSANGA SEKONDARI

N.B: SHULE HAITAPOKEA FEDHA TASLIMU.

ADA TSHS.70,000/= NUSU MUHULA TSH 35,000/=

1.	Tahadhari	5,000/= mara moja tu
2.	Kuboresha taaluma	20,000/= kwa mwaka
3.	Dawati	20,000/= mara moja tu
4.	Vibarua/Mpishi Mlinzi	30,000/= kwa mwaka
5.	Ukarabati	20,000/= kwa mwaka
6.	Matibabu	8,000/= kwa mwaka
7.	Mafuta ya Jenereta	5,000/= kwa mwaka
8.	Vifaa vya bweni	10,000/= kwa mwaka
	JUMLA	**118,000/=**

MUHIMU*:*

1. **RISITI YA BENKI IANDIKWE JINA LA MWANAFUNZI NA AJE NAYO SHULENI (NAKALA HALISI SI KIVULI):**

2. IFIKAPO MITIHANI YA TAIFA(NECTA), MOCK NA SERIES MZAZI ATAPASWA KUCHANGIA

BIDHAA ZIFUATAZO ZINAPATIKANA DUKA LA SHULE KWA BEI NAFUU

SN	BIDHAA	SN	BIDHAA
1	RIMU YA KARATASI=12,000	11	MKEBE WA HISABATI=
2	NDOO YA PLASTIKI =3000	12	TRACK SUIT ZA MICHEZO=25,000
3	MADAFTARI =3500	13	NETI ZA MBU=9000
4	GRAPH PAPER=3000	14	SANDUKU LA BATI=25000
5	KALAMU ZA WINO=200	15	SOKSI=1000
6	SWETA=15,000	16	KANDAMBILI=2000
7	SHUKA =10,000	17	MAPANGA=5000
8	T-SHIRT ZA KIJIVU=10,000	18	FYEKEO=4000
9	MPINI=2000	19	JEMBE=6000
10	SHATI NYEUPE ZA SHULE SHORT=9000/LONG SLEEVE =10,000	20.	SCIENTIFIC CALCULATOR-45,000/=

K: SHERIA ZA SHULE:

Shule inaendeshwa kwa Mujibu wa Sheria ya Elimu na: 25 ya mwaka 1978. Aidha miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

Sheria zote za shule zimewekwa ili kuwawezesha Wanafunzi kulifikia lengo la kuwepo kwao hapa shuleni bila matatizo. Aidha sote tunaelewa kuwa nidhamu nzuri huambatana na mafanikio mazuri kitaaluma pia.

1. **HESHIMA NA UTII**:

Wanafunzi wote hawana budi kuonyesha heshima mahali popote wanapokuwa shuleni na nje ya shule.

(i) Lugha chafu na matusi ni marufuku

(ii) Lazima wanafunzi kuheshimu na kuwatii viranja na viongozi wengine (iii) Wanafunzi hawana budi kupendana na kuheshimiana wao kwa wao.

(iv) Wanafunzi wawaheshimu na kuwatii walimu wote na wafanyakazi wasio walimu

(v) Ni lazima wanafunzi wawaheshimu Viongozi wote wa Taifa na Umma kwa ujumla.

(vi) Wanafunzi ni lazima kusabahi na kusalimu watu wengine kwa kadri ya hali wanayostahili. Wanafunzi wanalazimika kusimama na kusalimia kwa heshima walimu wao, wafanyakazi wasio walimu, wengine wanaoitembelea shule ikiwa ni pamoja na wakubwa wanaokutana nao mahali popote, ndani na nje ya shule.

(vii) Ni lazima kusimama mwalimu aingiapo darasani na kusalimia

Wanafunzi wanatakiwa kutii amri zitolewazo hapa shuleni na kuzingatia sana maagizo:

(i) Sehemu zifuatazo zitatembelewa kwa ruhusa maalum ya maandishi:

- Nyumba za wafanyakazi

- Hospitali, Posta, benki
- Maduka ya mjini Madizini
- Jengo la Utawala
- Ofisi za walimu
- Ukumbi wa Walimu (Staff room)

(ii) Ni marufuku kumruhusu Mgeni kufika eneo la Mabweni na kuingia Mabwenini. Hivyo basi mwanafunzi haruhusiwi kuongea au kupiga gumzo na mtu yeyote asiyekuwa Mwanajumuiya wa shule hii katika eneo lolote la shule bila kibali cha Mwalimu wa zamu. Kwa hiyo Mwanafunzi haruhusiwi kukaribisha au kupokea Mgeni wake nje ya utaratibu wa shule .

(iii) Ni marufuku mwanafunzi wa shule hii kuwa na simu ya mkononi. Mawasiliano kati ya Wazazi/Mzazi yatafanyika kupitia ofisi ya Mkuu wa Shule kwa simu zilizoonyeshwa kwenye Ukurasa wa 1.

(iv) Ni Marufuku kwa mwanafunzi kujihusisha na masuala ya mapenzi, kuwa na madawa ya kulevya na vileo vingine na kuvitumia au kuviuza.

(v) Ni marufuku kwa mwanafunzi kujihusisha na tabia za Usagaji.

(vi) Kila mwanafunzi anatakiwa kulala katika kitanda na bweni alilopangiwa muda wote awapo shuleni.

(vii) Ni marufuku kuunganisha umeme kwa namna yeyote maana wewe sio fundi umeme.

(viii) Ni marufuku kulala katika kitanda na bweni ambalo hujapangiwa

(ix) Vitu ambavyo mwanafunzi hatakiwi kujanavyo shuleni:

Simu, Radio, heater, camera, sigara, bangi, vileo vya aina yeyote, pasi ya umeme, manukato yoyote (*kwani yanaweza kusababisha magonjwa ya mfumo wa upumuaji*),vyakula vya aina yoyote.

MAHUDHURIO:

1. Kila Mwanafunzi ni lazima ahudhurie pale anapotakiwa bila kukosa wala kuchelewa.
2. Ni lazima Mwanafunzi awepo shuleni muda wote wa masomo
3. Ni lazima mwanafunzi awahi na kushiriki katika shughuli zote za shule kama kuitwa majina "Roll Call"
4. Ruhusa ya kuondoka shuleni kwa ajili ya shida nzito kama Msiba itatolewa na Mkuu wa shule au Makamu wake iwapo atakuwa hayupo Mkuu wa shule.
5. Ruhusa ya kwenda Hospitali itatolewa na Matroni au muuguzi wa shule baada ya kumwona mwanafunzi mgonjwa akishirikiana na mwalimu wa zamu na Mlinzi
6. Mzazi/Mlezi aliyeandikishwa shuleni ndiye anayeruhusiwa kumwombea mwanafunzi ruhusa kila itakapolazimu kufanya hivyo na sio vinginevyo; au kumtembelea shuleni siku zilizopangwa.

UVAAJI WA SARE NA UNADHIFU:

1. Vazi rasmi la shule huvaliwa wakati wote Wanafunzi wakiwepo shuleni na penginepo kwa shughuli za kielimu/kishule na pia mwanafunzi aendapo au kurudi shuleni wakati wa kwenda au kutoka likizo.
2. Hereni, bangili, vipini, kofia, shanga, miwani ya jua , mikufu na pete za aina yoyote havitaruhusiwa kuvaliwa shuleni.
3. Nywele: Mwanafunzi HATARUHUSIWA kusuka. Atakata nywele wakati wote.
4. Usipake wanja, shedo, lip bum wala kutinda nyusi. Mdomo ukikauka upakwe mafuta ya mgando.
5. Ni marufuku kupunguza urefu wa sketi na kubana upana wa sketi uliyoshonewa.

MWANAFUNZI AKITENDA MAKOSA AU MOJAWAPO YA MAKOSA YAFUATAYO ANAWEZA KUFUKUZWA SHULE.

. Wizi

. Utoro (Kukaa nje ya shule bila taarifa kwa zaidi ya siku 90)

. Uasherati/Usagaji
Kutoa lugha chafu shuleni

. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya .

. Uvutaji bangi.

. Makosa ya Jinai

. Kupigana au kupiga

. Kuharibu kwa makusudi mali ya Umma

. Kudharau bendera ya Taifa

. Kuolewa

. Kupata mimba .
Kutoa mimba

. Kugoma, Kuchochea na kuongoza migomo au kuvuruga amani na usalama wa
Jumuiya ya shule

. Kukaa vikao visivyo rasmi katika eneo la shule

. Kukataa adhabu itolewayo na mwalimu

. Kuwa na simu au line ya simu

- Kujibizana,kumtukana au kuonyesha dharau kwa mwalimu au mfanyakazi mwingine wa shule
- Kuwa na uhusiano ya kimapenzi kati ya mwanafunzi na mwanafunzi, mwanafunzi na mwalimu au mwanafunzi na mfanyakazi mwingine wa shule

MWISHO:

Hakikisha unafika shuleni tarehe 03/07/2021 kama ilivyopangwa . Usipofanya hivyo, wala kutoa taarifa ya kutofika utahesabiwa kuwa hutafika na nafasi itarudishwa katika Mamlaka husika za uchaguzi ili nafasi hiyo wazi iweze kuchukuliwa na Mwanafunzi mwingine.

Aidha tarehe ya Mwisho kabisa Kuripoti shuleni ni 18/07/2021

Ninachukua nafasi hii kukukaribisha tena Lusanga Sekondari na ni matarajio yangu kuwa u taitumia vyema nafasi hii uliyotunukiwa na Taifa lako.

(Bahati M. Omary)
MKUU WA SHULE

KWA MSAADA ZAIDI WASILIANA:
1.OFISI YA MAKAMU MKUU WA SHULE
0715524058
0712408806

2.**OFISI YA MALEZI**
0625072365
0719889912

NAMBA ZA MAWASILIANO NA MWANAFUNZI AWAPO SHULENI
1.OFISI YA MALEZI
0719669477
0756361306

2.**OFISI YA MATRON**
0719672919
0756739786

OFISI YA RAIS - TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
SHULE YA SEKONDARI LUSANGA

FOMU YA TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI NA KUKUBALI SHERIA NA NAFASI YA SHULE ALIYOPEWA

A: TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI

- JINA LA MWANAFUNZI …… - TAREHE YA KUZALIWA……
- MAHALI ALIPOZALIWA (MKOA/ WILAYA) ……
- MAHALI ANAPOISHI (KATA/MTAA) .....
- URAIA ……. - SHULE ALIYOTOKA…….
- NAMBA YA MTIHANI/USAJILI……..

B: TAARIFA YA MZAZI:

- JINA LA MZAZI/MLEZI ……
- KAZI YA MZAZI/MLEZI …… - ANUANI YA MZAZI/MLEZI ……..
- SIMU YA MZAZI/MLEZI (tafadhali andika namba zinazotumika na mhusika kama ni mama au baba n.k)……

C: KUKUBALI NAFASI NA MAELEKEZO ULIYOPEWA (MWANAFUNZI)

Mimi ……. Kidato ……mwaka…… Nimesoma na kuyaelewa yote. Kwa hiyo nakubali kuipokea/sikubali kuipokea nafasi niliyopewa. Nathibitisha kwamba nimepokea maagizo au maelekezo bila kulazimishwa kuyazingatia.

Tarehe ……. Sahihi ……

D: **KUKUBALI SHERIA ZA SHULE :(MWANAFUNZI)**

Mimi …… nimezisoma na kuzielewa sheria za shule na naahidi kwamba nitazingatia na kutii masharti, sheria za shule na maelekezo mengine nitakayopewa na walimu na viongozi wote wa shule, nikikiuka sheria hizo hatua za kinidhamu zichukuliwe dhidi yangu kwa mujibu wa kanuni, taratibu na sheria zilizopo.

Tarehe …… Sahihi …….

E: MZAZI/MLEZI – (Ajaze sehemu hii)

(i) Mimi Mzazi/Mlezi wake nathibitisha kuwa Mwanangu (jina la

mtoto)…….…… ameelewa maagizo na ninapenda ifahamike kuwa dini ya mwanangu ni…… dhehebu lake ni …….

(ii) Ninaruhusu/Siruhusu (kata isiyohusika) mwanangu kushiriki katika Makongamano au Warsha za kidini nje ya shule zinazofanyika nje ya Mkoa wa Morogoro pasipo na Mwalimu wa shule hii.

(iii) Ninaruhusu/Siruhusu (kata isiyohusika)wakati wa likizo fupi(mid-term) atoke shuleni na kwenda kwa……wa (mahali)…… Uhusiano wake na Mwanangu ni ……Namba yake ya simu ni ……

(iv) Ninaruhusu wafuatao wamtembelee mwanangu siku maalum ya kuona wanafunzi

(1) ……...(anakoishi)…… … …(simu)…….....

(2) …… …… .(anakoishi)……..…. ..(Simu)…….……

(3) …….....(anakoishi)……..(simu)……...

MUHIMU: **kutembelea mwanafunzi ni jumamosi ya mwisho wa kila mwezi**, tofauti na hapo hutopokelewa.
Pia mwanao ataruhusiwa kwenda likizo fupi kwa mtu au mahali ulipoelekeza wewe hatutapokea mabadiliko kulingana na maelekezo ya mwanafunzi.

(v) Aidha mimi …….. ambaye ni Mzazi/Mlezi, nimesoma/nimesomewa sheria na maagizo mengine ya shule yanayomhusu mwanafunzi (jina la mwanafunzi)……na kuahidi kutimiza wajibu wangu nikiwa Mzazi/Mlezi wa mtoto huyu kwa kumshauri ipasavyo pamoja na kumtimizia mahitaji yake ya shule.

…….…… **……...**
JINA LA MZAZI/MLEZI ***SAHIHI YA MZAZI/MLEZI***

……..……...

TAREHE

F. SEHEMU YA NDUGU WA KARIBU

Ndugu wa karibu wanaoruhusiwa kumtembelea mtoto: BABA MAMA

JINA UHUSIANO

1..... .....

2..... .....

3..... .....

4..... .....

5..... .....

MLEZI -01 MLEZI-02 MLEZI-03

G. KIKAO CHA WAZAZI

Kitafanyika mara moja kwa mwaka wa masomo 2021/2022.Wazazi/walezi mtaarifiwa siku na tarehe ya kikao hicho.

Masharti mahususi:

1. Ni lazima mzazi/mlezi kuhudhuria kikao
2.Udhuru wowote hautakubalika
3.Kwa mzazi/mlezi asiyefika siku ya kikao atalipa faini ya shilingi elfu hamsini (50,000) Vinginevyo mwanafunzi hatapokelewa na atalazimika kurudi alikotoka

H. SEHEMU YA MZAZI KUKIRI KUHUDHURIA KIKAO CHA WAZAZI

Mimi.....mzazi wa .....wa kidato cha .....

Nitahudhuria kikao cha wazazi bila kukosa hapo shuleni kwa tarehe itakayopangwa

....

Sahihi Tarehe

KARIBU SANA LUSANGA SECONDARI

.....

Bahati M. Omary

MKUU WA SHULE

MKUU WA SHULE
SHULE SEKONDARI LUSANGA
S. L. P. 150, TURIANI

PRESIDENT'S OFFICE REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENTS
REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

PART A **From: The Headmistress**

Lusanga Secondary School,
P.O. Box 150,
Turiani - Morogoro

To

The Medical officer,

……

……

…….. (Name of student in full) Please examine the above named student as to her physical and mental fitness for a full time student. The examination should included the following categories (a-d)

(a) (i) Eyesight (ii) Hearing (iii) Speech (iv) Venereal disease (v) Limbs
(vi) Leprosy (vii) Epilepsy
(b) Neurosis
© Other serious diseases eg. Asthma, Tb etc
(d) Pregnancy

Name: Bahati M. Omary Date: 03th May 2021 Signature.

MKUU WA SHULE
SHULE SEKONDARI LUSANGA
S. L. P. 150, TURIANI

PART B: MEDICAL CERTIFICATE

(To be completed by a Government Medical Officer) I have examined the above student and consider that she is fit/unfit for full time studies.

(i) Eyesight……..
(ii) Hearing…… (iii) (iii)
Speech ……. (iv)
Limbs…… (v)
Venereal diseases……..
(vi) Leprosy ……
(vii) Epilepsy……
(viii) Neurosis……
(ix) Other serious eg. Asthma ……
(x) T.B……
(xi) Pregnancy ……

Other Comment ……
Name …….. Date ……..…… Signature ……..

STATION ……. DESIGNATION ……

LIST OF BOOKS.

1. ENGLISH LANGUAGE/LITERATURE
    - AN INTODUCTION TO LINGUISTIC, LANGUAGE GRAMMA & SEMANTICS (20070 BY JINDAL. D.
    - AN INTRODUCTION TO LANGUAGE (2007).BY FROMKIN. V
    - ADVANCED ENGLISH LANGUAGE 5&6 (200100. BY JOHN, J. OXFORD
    - ADVANCED LEVEL ENGLISH.A PRACTICAL APPROACH (2010) BY NICHOROUS, ASHERI.
    - ADVANCED LEARNER'S DICTIONARY (COMPULSORY)

    - **NOVELS:**
      A MAN OF THE PEOPLE
      BEAUTIFUL ONES ARENOT YET BORN
      HIS EXCELLENCY HEAD OF STATE
      SEASON OF WAITING

    - **PLAY:**
      AN ENEMY OF THE PEOPLE
      BLACK MAMBA
      BETRAYAL IN THE CITY
      I WILL MARRY WHEN I WANT

    - **POETRY**
      ENCOUNTER FROM AFRICA
      SELECTED POEMS FROM EAST AFRICA

    AT LEAST 2 BOOKS IN EACH CATEGORY

2. KISWAHILI SARUFI/FASIHI
    - NADHARIA YA LUGHA KIWAHILI 1 KIDATO CHA 5&6 (2016). J.A MASEBO & NYANGWINE
    - NADHARIA YA FASIHI KISWAHILI 2 KIDATO CHA 5&6 (2016). J.A. MASEBO & NYANGWINE.
    - SAMIKISA (SARUFI MIUNDO) MASAMBA NA WENZAKE
    - SAMAKISA (SARUFI MAUMBO)
    - VUTA N' KUVUTE (SHAFII A. SHAFII)
    - KAMUSI

3. HISTORY
    - AFRICA FROM NEOLITHIC REVOLUTION TO PRESENT (ZISTI KAMILI) 2012
    - CONTEMPORARY HISTORICAL EVENTS ADVANCED LEVEL HISTORY ONE (COMRADE SHIBITAL C.K. TUMAINI)
    - HOW EUROPE UNDERDEVELOPED AFRICA (WALTER RODNEY 2001)
    - MASTERING MODERN WORLD HISTORY (HAMPSHIRE PALGAVE. NORMAL LOWE 1997)
    - THE MODERN WORLD SINCE 1870, (LONGMAN GOUP LTD, HONGKONG)
    - A HISTORY OF AFRICA VOL.1 (ASSA OKOTH 1915-1995)
    - NOMAN LOWE (20130 MASTERING MODERN WORLD HISTORY

- PEACOEK (1982) 7TH EDITION: THE HISTORY OF MODERN EUROPE FROM 1789 – 1981.

4. GEOGRAPHY
    - DAVID WAUGH & NELSON THORNES (2009/ANY), GEOGRAPHY AN INEGRATED APPROACH,4TH EDITION, PRINTING INTERNATIONAL LTD.
    - COLIN BUCKLE (1978) LANDFORMS IN AFRICA, AN INTRODUCTION TO GEOGRAPHY, LONGMAN GROUP LTD
    - JOHN M. PRITCHARD (1984), PRACTICAL GEOGRAPHY FOR AFRICA.LONGMAN GROUP LTD.
    - R.B. BURNET (1988), PHYSICAL GEOGRAPHY IN DIAGRAS FOR AFRICA. LONGMAN GROUP LTD HONGKONG.
    - COTHARI (2013), RESEARCH METHODOLOGY
    - GOH CHENG LEONG & GILLIAN C. MORGAN (1973), HUMAN ECONOMIC GEOGRAPHY, 2ND EDITION, OXFORD UNIVERSITY PRESS.
    - KIBUUKA P. KARUGGAR & MUGO M. (20050.CERTIFICATE GEOGRAPHY FORM 4. OXFORD UNIVERSITY PRESS.

5. BASIC APPLIED MATHEMATICS
    - BASIC APPLIED MATHEMATICS FOR ADVANCED LEVEL SECONDARY SCHOOLS (TIE)
    - BASIC APPLIED MATHEMATICS FOR ADVANCED LEVEL BY RESPICIUZI KIIZA & LUGANO MWANGINDE.
    - BASIC APPLIED MATHEMATICS FOR ADVANCED SECONDARY SCHOOLS BY SEPTINE INYASI SILLEM.
    - BASIC APPLIED MATHEMATICS REVIEW BOOK FOR PROBLEMS AND SOLUTIONS 1998 – 2013 BY IMMACULATA MOSHA & YAHYA KAWIA.

6. BIOLOGY
    - BIOLOGICAL SCIENCE (BS)
    - BIOLOGY FUNCTIONAL APPROACH
    - UNDERSTANDING OF BIOLOGY

7. CHEMISTRY
    - MODERN'S ABC OF CHEMISTRY CLASS XI – PAT I & II.DR.S.P. JAUHAR
    - ADVANCED LEVEL PHYSICAL CHEMISTRY WITH GENERAL CHEMISTRY (APE NETWORK). MARK DANIEL & HERMES DARMIANS.
    - CONCEPTUAL CHEMISTRY FOR CLASS XI.S. CHAND
    - GENERAL CHEMISTRY FOR ADVANCED LEVEL SECONDARY SCHOOLS STUDENT'S BOOK. FIVE & SIX. (TIE)
    - PHYSICAL CHEMISTRY FOR ADVANCED LEVEL SECONDARY SCHOOLS STUDENT'S BOOK. FORM FIVE & SIX(TIE)
    - ORGANIC CHEMISTRY FOR ADVANCED LEVEL SECONDARY SCHOOLS STUDENT'S BOOK. FORM FIVE & SIX. (TIE)
    - INORGANIC CHEMISTRY FOR ADVANCED LEVEL SECONDARY SCHOOLS STUDENT'S BOOK.FORM FIVE & SIX.

8. PHYSICS
    - A-LEVEL PHYSICS BY ROGER MUNCASTER 4TH EDITION
    - NEW UNDERSTANDING PHYSICS FOR ADVANCED LEVEL 4TH EDITION
    - PHYSICS FOR ADVANCED LEVEL BY TIE
    - CHAND'S PRINCIPLE OF PHYSICS FOR CLASS XI OR XII
    - SCIENTIFIC CALCULATOR (COMPULSORY) AVAILABLE AT SCHOOL

9. GENERAL STUDIES
    - KAMILI ZISTI (2017). GENERAL STUDIES ALIVE.A STRAIT FORWARD GENERAL & DEVELOPMENT STUDIES FOR HIGH SCHOOLS & UNIVERSITY STUDIES.DAR ES SALAAM KAMILI BOOKS & GENERAL SUPPLIES.(THE BEST BOOK)
    - BIGIRWAMUNGU J & DEOGRATIAS S (2018). UNDERSTANDING GENERAL STUDIES FOR ADVANCED LEVEL.DAR ES SALAAM. AFRICA PROPER EDUCATION NETWORK.